TANGAZO LA SERIKALI Na. 691 La Tarehe 25/11/2022

# SHERIA YA MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI,
(SURA YA 414)

## NOTISI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 19 (4))*

NOTISI YA MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (TAFTISHI KUHUSU MAOMBI YA BEI ZA MAJI YA MAMLAKA YA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA MBEYA (MBEYA WSSA), 2022

Jina

1. Notisi hii itajulikana kama Notisi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (Uchunguzi kuhusu Maombi ya Bei za Maji ya Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Mbeya) (Mbeya WSSA) la Mwaka 2022.

Tafsiri

2.Katika Notisi hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

Sura Na. 414

"Mamlaka" inamaanisha Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji iliyoanzishwa na Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji;

"Mkurugenzi Mkuu" inamaanisha Afisa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka;

"Ombi la Marekebisho ya Bei" ina maanisha ombi la kurekebisha bei za huduma za maji kama inavyooneshwa kwenye majedwali ya Notisi hii; na

"uchunguzi" inamaanisha mchakato mzima wa kupokea maoni kutoka kwa wadau kuhusu marekebisho ya bei yanayopendekezwa kama inavyooneshwa kwenye majedwali.

Madhumuni ya uchunguzi

3. Madhumuni ya huu uchunguzi ni kuiwezesha Mamlaka kukusanya maoni ya wadau kuhusu bei zinazopendekezwa.

Mapendekezo la bei

4. Bei zinazo pendekezwa na Mbeya WSSA zimeoneshwa kwenye majedwali ya Notisi hii.

Jinsi ya kushiriki katika uchunguzi

5. Mtu yeyote anayetaka kushiriki kwenye uchunguzi anaweza kufanya hivyo kwa kuwasilisha maoni yake kuhusiana na suala hilo kwa maandishi kwa Mkurugenzi Mkuu kupitia anuani iliyotajwa katika aya ya 9 ndani ya siku kumi na nne (14) tangu kuchapishwa kwa Notisi hii.

Pingamizi

6. Mtu yeyote anayekusudia kupinga uidhinishwaji wa bei atawasilisha pingamizi lake kwa maandishi ndani ya siku tano za kazi tangu siku ya kuchapishwa kwa Notisi hii.

Nakala za maombi

7. Nakala za maombi zinapatikana kwenye Ofisi za Mamlaka wakati wa saa za kazi kuanzia saa 3.00 asubuhi hadi saa 10.00 jioni kwa ajili ya taarifa kwa umma. Maelezo ya zaidi yanaweza kupatikana kupitia maombi ya maandishi kwa Mkurugenzi Mkuu kupitia anuani iliyotajwa kwenye aya ya 9 ya Notisi hii.

Anwani ya Mamlaka

8. Anuani ya Mamlaka itakuwa:
Mamlaka ya Udhibiti waHuduma za Nishati na Maji,
Jengo la EWURA, Kiwanja Na.3, Kitalu AD,
Medeli Magharibi,
S.L.P. 2857,
DODOMA

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 4)*

Bei za sasa na zinazopendekezwa (Shilingi kwa mita moja ya ujazo)

| Kundi la Wateja | Matumizi ($m^3$) | Bei za Sasa | Bei Zinazopendekezwa | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 |
| Majumbani | 0-10 | 1,100 | 1,251 | 1,518 | 1,675 |
| | >10-20 | 1,100 | 1,558 | 1,684 | 1,937 |
| | >20 | 1,300 | | | |
| Taasisi | 0-30 | 1,500 | 2,652 | 2,956 | 2,956 |
| | >30 | 1,700 | | | |
| Biashara | 0-30 | 1,500 | 1,916 | 2,135 | 2,135 |
| | >30 | 1,700 | | | |
| Viwanda | 0-50 | 1,700 | 3,228 | 3,368 | 3,509 |
| | >50 | 1,900 | | | |
| Vioski | | 1,000 | 2,500 | 2,500 | 2,500 |
| Boza la Maji | | 2,700 | - | - | - |

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 4)*

Ada za Sasa na Zinazopendekezwa za Kurejeshewa Hudumaya Maji Baada ya Kusitishwa (Shilingi kwarejesho)

| Kundi la Wateja | Bei za Sasa | Bei Zinazopendekezwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 |
| Majumbani | 20,000 | 20,000 | 20,000 | 20,000 |
| Taasisi | 30,000 | 30,000 | 30,000 | 30,000 |
| Biashara | 30,000 | 35,000 | 35,000 | 45,000 |
| Viwanda | 40,000 | 45,000 | 50,000 | 50,000 |

JEDWALI LA TATU

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 4)*

Ada za Sasa na Zinazopendekezwa za Maunganisho Mapya (Shilingi kwa maunganisho mapya)

| Kundi la Wateja | Ada ya Sasa 2021/22 | Ada zinazopendekezwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 |
| Majumbani | Asilimia 20 ya Gharama za Vifaa na Nguvu kazi kama ilivyoainiswa katika Sehemuya 24 ya Kanuni za Maji 2013 | Asilimia 20 ya Gharama za Vifaa na Nguvu kazi kama ilivyoainishwa katika Sehemu ya 26 ya Kanuni za Maji 2019 | | |
| Taasisi | | | | |
| Biashara | | | | |
| Viwanda | | | | |

JEDWALI LA NNE

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 4)*

Bei za Sasa na Zinazopendekezwa za Majitaka kwa Wateja wenye Majisafi
(Shilingi/Mita Moja ya Ujazo)

| Kundi la Wateja | Bei za Sasa | Bei zinazopendekezwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 |
| Majumbani | 385 | 420 | 450 | 500 |
| Taasisi | 500 | 550 | 600 | 660 |
| Biashara | 575 | 630 | 690 | 760 |
| Viwanda | 700 | 770 | 850 | 940 |

JEDWALI LA TANO

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 4)*

Bei za Sasa na Zinazopendekezwa za Majitaka kwaWateja Wasio na Maunganisho
ya Majisafi ya Mamlaka (Shilingi/Mwezi)

| Kundi la Wateja | Bei za Sasa | Bei Zinazopendekezwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 |
| Majumbani | 20,000 | 22,000 | 22,500 | 23,000 |

| Kundi la Wateja | Bei za Sasa | Bei Zinazopendekezwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 |
| Taasisi | 24,000 | 25,000 | 30,000 | 50,000 |
| Biashara | 36,000 | 45,000 | 50,000 | 55,000 |
| Viwanda | 36,000 | 40,000 | 43,000 | 45,000 |

JEDWALI LA SITA

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 4)*

Bei za Sasa na Zinazopendekezwa za Kunyonya Majitaka
(Shilingi kwa Safari Moja)

| Kundi la Wateja | Bei ya Sasa | Bei Zinazopendekezwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 |
| Majumbani | 50,000 | 50,000 | 50,000 | 50,000 |
| Taasisi | 50,000 | 75,000 | 75,000 | 100,000 |
| Biashara | 50,000 | 75,000 | 75,000 | 100,000 |
| Viwanda | 50,000 | 75,000 | 75,000 | 100,000 |

Dodoma,
24 Novemba, 2022

MODESTUS M. LUMATO,
*Director General*